



NY State of Health ni soko la Mpango Rasmi wa Afya wa New York.

Ikiwa una miaka 19 au zaidi na unaishi New York State, tunaweza kukusaidia kupata bima ya afya katika gharama unayoweza kuimudu.

Je, nitajisajili vipi?

☞ nystateofhealth.ny.gov
AU

☞ **1-855-355-5777 au TTY:
 1-800-662-1220**
AU

☞ **Kupitia usaidizi wa ana kwa ana wa bila malipo kutoka kwa msaidizi aliyeidhinishwa karibu na nyumbani au kazini kwako.**

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

Bima ya Afya kwa kwa Watu Wazima Wadogo

Hapa kuna vitu 4 muhimu unavyopaswa kuvijua

1 Una machaguo

Kama mtu mzima mdogo, unapaswa kuamua ikiwa utasalia kwenye bima ya afya ya wazazi wako. Ikiwa utaamua kupata bima yako mwenyewe, utapata machaguo mengi katika NY State of Health. Kuna mipango mingi kwa viwango tofauti vyta vifurushi na masharti ya malipo. Hii humaanisha huenda ukapata ambayo hukudhi mahitaji yako na kuwa ndani ya bajeti yako.

2 Utapata bei nzuri

Bila kujali gaharama yake, bima zote za afya zinazotolewa NY State of Health lazima zishughulikie huduma za afya 10 muhimu. Hizi hujumuisha dawa za kuandikiwa, kumwona daktari, huduma za hospitali na huduma za dharura – hata huduma za uzuaijji na ustawi. Kwa hiyo utapata dili zuri, haijalishi ni bima gani ya afya utakayoichagua.

3 Bima za bei nafuu zinapatikana

Kwa wale wanaokidhi vigezo, Medicaid na Essential Plan wanatoa bima yenye ubora unaofanana na bima nyingine kwa bei ya chini au bila gaharama kwa kila mwezi. Medicaid haina malipo ya juu au makato na malipo ya gaharama ya chini; Essential Plan ina gharama ya chini ya dola moja kwa siku, haina makato na malipo ya gharama ya chini. Kwa bima nyingine zote, tazama kuangalia iwapo unakidhi vigezo ya kupata usaidizi wa kifedha ili kushusha gharama zako.

4 New York State imefanya iwe rahisi kununua na kulipia bima ya afya

Kwa watu wengi zaidi, bima humaanisha mikataba mingi na mikanganyiko. Tunapata hiyo. Kwa hiyo tumewaweka wataalamu wengi wenye mafunzo kwenye kesi ili kukusaidia, hatua kwa hatua, kupitia kuchagua na kujisajili kwenye bima ambayo inakufaa. Unaweza kupata usaidizi mtandaoni, kwenye simu au ana kwa ana katika jamii yako. Pia inapatikana katika lugha nyingi.